The Baptist Tabernacle of Los Angeles

1329 South Hope Street, L.A. Civic Center

Mailing Address:
P. O. Box 15308
Los Angeles, CA 90015
Phone: (213) 744-9999
E-mail: rlhymersjr@sbcglobal.net
www.sermonsfortheworld.com
www.baptisttabernacle.com

Dr. R. L. Hymers, Jr.
Senior Pastor

Dr. Christopher L. Cagan
Associate Pastor

Desemba, 2018

Rafiki Mpendwa:

"Dhidi Ya Woga Yote" ni hadithi ya maisha yangu, iliyochapishwa Aprili mwaka huu. Mmoja kati ya wale waliokisifu kitabu changu ni Dkt. Bob Jones III, aliyesema kwamba mimi ni kama "nabii wa Agano la Kale." Dkt. Bill Monroe, aliyekuwa rais wa BBF mara mbili, alisema, "Hymers ni Danieli wa siku hizi." Na Dkt. Herbert Rawlings, mwana wa kiume wa mwanzilishi wa BBF Dkt. Yohana Rawlings, mkuu wa wakfu wa Rawlings, aliniita, "Mmarekani asili! Mwenye maono! Shauku ya maisha yake ni -- kufanikisha matakwa ya Kristo." Mwinjilisti Don Boys alisema, "'Dhidi Ya Woga Wote' ni kitabu kinachostahili kusomwa na watu wote, si wahubiri pekee. Hymers ni mfano wa kila mtu…Hadithi yake inaangazia hitaji la wakati huu – ujasiri, kujitolea, na nidhamu."

Ninaposikia Wakristo hawa mashuhuri wakiongea kunihusu kwa namna hii, wakati mwingine nashangaa ilivyotendeka. Mara kwa mara ushangaa, "Nimekuwa mtu wa namna hii kwa jinsi gani?" Mapema katika huduma yangu, hata kabla sijaitwa kuhubiri, Mungu alinipa mstari wangu wa maisha,

"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13).

Kwa karibu miaka 61 nimepata ahadi hii kuwa kweli. Katika maisha yangu yote nimekumbana na changamoto nyingi na vizuizi. Lakini nimeshinda kila vita kwa sababu kila wakati nimemtegemea Yesu Kristo. Kwa sababu ya Kristo nimevuka vizuizi vya ajabu na kuwa kielelezo kwa mamilioni ya watu katika ulimwengu. Nimeshinda kila vita kwa sababu nimemtegemea Yesu Kristo kabisa.

Ifuatayo ni baadhi tu ya vita "vikubwa". Kulikuwa na <u>vita kuonyesha kwamba Biblia haina kasoro</u>, ambapo nilisimama kinyume na mafundisho ya uongo katika seminari niliyosomea iliyodhalilisha mandiko. Nilishinda hivyo vita kwa sababu nilimtegemea Kristo kabisa. Halafu kulikuwa <u>na vita dhidi ya filamu bovu inayokufuru Mungu</u>, "Jaribu la Mwisho la Kristo," filamu iliyomwonyesha Yesu akijamiiana na Mariamu Magdalene. Nilishinda vita hivyo kwa sababu nilimtegemea Kristo kabisa. Habari za "uongo" katika runinga na magazeti zilinilaumu kuwa nina chuki dhidi ya wayahudi. Nilishinda vita hivyo, na kabisa niliondolewa yale mashtaka, kwa sababu nilimtegemea Yesu Kristo, na Yeye pekee. Halafu kulikuwa <u>na vita dhidi ya uavyiaji wa mimba</u>. Kasisi. Yohana Samweli Cagan, msaidizi wangu, alisema, "Dkt. Hymers aliliongoza kanisa lake katika vita vya kufunga zahanati mbili za uavyiaji wa mimba. Hakuacha vita hivyo hadi zahanati hizo mbili zikafungwa." Nilisimama na Yesu, na tulishinda vita kwa sababu tulimtegemea Kristo. Halafu <u>kulikuwa na vita vya kuokoa jengo la kanisa letu</u>. Mtu mwovu na mwenye dhambi aliwachukua washirika 320 wa kanisa letu na tulikuwa karibu kupoteza jengo la kanisa letu. Tuliweza kushinda vita hivyo pia, kwa sababu "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." Ninapokuwa kwa vita aina hii, huwa natafakari ni upande upi ulio sawa na ni upande upi usio sawa. Halafu najiunga na upande ulio sawa, na kila mara nashinda kwa sababu " Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

Wakati huu, ambapo wahubiri wengi wanajaribu kuongeza idadi katika makanisa yao kwa kuwaiba washirika kutoka kwa makanisa mengine, sikuwa na haja ya kufanya hivyo kwa sababu niliweza kuwafikia watu waliopotea katika ulimwengu. Kwa nini? Kwa sababu "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." <u>Hiyo ndiyo sababu</u>! Hiyo ndiyo sababu tulishinda vita vya kupeleka Injili kote ulimwenguni. Leo watu milioni 1.5 husoma mahubiri yangu kupitia tovuti yetu katika zaidi ya nchi 221 katika ulimwengu, kwa lugha 40 – kwa sababu "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

Kasisi. Yohana Cagan alisema, "Dkt. Hymers anajua kupitia ozoefu wa muda mrefu kwamba njia thabiti ya mtu kutumia kuyajenga maisha yake ni Mwamba Imara – Kristo Yesu."

Mwanangu wa kiume Robert alisema, "ni watu wachache tu wamemuelewa babangu, kwa sababu afikirii kama mtu wa kawaida. Yeye hutembea na Mungu." Nimeshinda kila vita ambavyo nimepigana kwa sababu ya jambo

TOVUTI YETU INATOA MAMIA YA MAHUBIRI NENO-KWA-NENO KWA LUGHA AROBAINI KUPITIA WWW.SERMONSFORTHEWORLD.COM.

hili moja – “Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Hiyo ndiyo sababu tuna hili kanisa. Hiyo ndiyo sababu, nilipouliza walioongoka kupitia mahuri yangu wasimame, karibu kila mtu alisimama. Ni watu wawili tu waliongokea mahali pengine.

Mshiriki wangu mwaminifu na rafiki, Dkt. Christopher L. Cagan, alisema, “Dkt. Hymers ni mtu aliyejikwaa, aliyechubuliwa na kuvunjika, aliyeinuka na kushinda vizuizi vikubwa kuonyesha watu kwamba Yesu Kristo anaweza kuwasaidia pia.”

Dkt. Edi Purwanto alisema, “Mungu anapokuwa na mtu, hawezi kushindwa.”

Dkt. Robert L. Sumner alisema, “Napongeza na kupendezwa na mtu aliyetayari kusimama kwa ajili ya ukweli, hata ingawa mambo yote yako kinyume na yeye. Robert Leslie Hymers, Jr. ni Mkristo wa namna hiyo.”

Dkt. Kent Philpott alisema, “Dkt. Hymers ndiye mhubiri bora kabisa kila mmoja wetu amewahi kumsikiliza, ‘mhubiri halisi wa kale.’ Lengo lake limekuwa kila wakati [kwa] ujumbe wa Kristo.”

Dkt. Neal Weaver alisema, “Dkt. Hymers ni mtu mwenye ujasiri, aliye na dhamiri madhubuti, na yuko [tayari] kupigania dhana hii dhidi ya pingamizi zote.”

Dkt. Phil Goble alisema, “...mfuate huyu mhubiri mashuhuri katika ulimwengu unaopingana na ukristo na tupigane kama yeye, vita vizuri vya imani.”

Dkt. Christopher L. Cagan alisema, “Dkt. R. L. Hymers, Jr. ni mtu ambaye amefaulu katika mambo magumu – dhidi ya woga wote! Ninajua, kwa sababu nimefanya kazi naye kwa zaidi ya miaka arobaini.”

Unaweza kupata nakala ya wasifu wangu, “Dhidi Ya Woga Wote,” kwa $10.00 pekee. Mwandikie Dkt. C. L. Cagan kupitia anwani hii, S.L.P. 15308, Los Angeles, California 90015. HAKIKISHA UMEANDIKA MANENO “BARUA YA KRISMASI” KATIKA HUNDI YAKO NA UTAPUNGUZIWA $10.00. Tuma $10.00 na utapata hadithi ya maisha yangu!

Nitaomba Mungu akubariki wakati wa Krisimasi. Na Mungu akubariki mwaka mpya pia! HebuYesu Kristo atukuzwe!

Dkt. Hymers pamoja na mke wake Ileana, mwana wake wa kiume Robert, na Jin mkewe Robert, na watoto wawili wa kike wa Robert, Hana na Sara.

Ndimi wako katika Yesu,

R. L. Hymers, Jr.,
D.Min., Th.D., Litt.D.
Wafilipi 4:13

Jamii ya Hymers pamoja na mjombake mke wa Hymers Francisco Castro, Carolina, Briana, kutoka Guatemala, Erwin Cuellar na Antione.

Dkt. na Bi. Hymers wakiwa na Dkt. Elmer L. Towns, aliyefundisha siku ya wafanyikazi mwisho wa juma.

TOVUTI YETU INATOA MAMIA YA MAHUBIRI NENO-KWA-NENO KWA LUGHA AROBAINI KUPITIA WWW.SERMONSFORTHEWORLD.COM.